MCHAKATO WA WANAODAI UKIMBIZI CANADA

Chini ya sheria za uhamiaji Canada, mtu aliye Canada anaweza kudai hadhi kama mkimbizi wa mkataba au mtu anayehitaji ulinzi.

Wakimbizi wa Mkataba ni watu ambao wako nje ya nchi yao na walio na hofu ya mateso kwa sababu ya ujamii, dini, maoni ya kisiasa, utaifa, au tarifa ya kijamii.

Watu Wanaohitaji Ulinzi ni watu wanaokabiliwa na mateso, hatari kwa maisha, ama ukatili na matendo yasiyo ya kawaida au adhabu, wakirudi nchi yao ya kitaifa au makao.

Nchi Teule za Asili (DCO)

Mdai wa Ukimbizi anaweza kupangwa kama mtu anayetoka Nchi Teule ya Asili. Wadai wa Ukimbizi kutoka Nchi Teule za Asili wanafaa kufahamu kuwa kuna muda tofauti na wale wanaodai kutoka Nchi Teule za Asili.

Ni muhimu kwako kujua kama nchi yako iko kwa orodha ya Nchi Teule za Asili. Kujua kama nchi yako imeorodheshwa, enda http://www.cic.gc.ca/english/refugees/reform-safe.asp

Ukihitaji msaada juu ya swala hili, tafadhali piga simu kwa mpango wa Mawasiliano ya Kwanza na mtu wa kujitolea ataweza kukusaidia.

Wakala Muhimu za Serikali

Wakala hizi 3 za Serikali zinahusika moja kwa moja wakati wa mchakato wa madai yako. Ukibadilisha anwani yako au nambari ya simu, lazima uwasiliane na kila wakala kibinafsi na maelezo yako mapya.

Bodi ya Uhamiaji na Ukimbizi- Idara ya Ulinzi wa Wakimbizi (IRB-RPD)

- Hukagua Fomu ya Msingi wa Madai yako (BOC)
- Hufanya usikizi wa kesi yako ya ukimbizi
- HiHHuamua kama madai yako ya ukimbizi yamekubaliwa au yamekata-liwa

Mawasiliano:

Library Square, 16th Floor
300 West Georgia Street
Vancouver BC V6B 6C9

Phone: 604-666-5946 or 1-866-787-7472
Fax: 604-666-3043
Website: www.irb-cisr.gc.ca

Wakala wa Huduma ya Mpaka wa Canada (CBSA)

- Huamua kama unaweza kufanya madai katika Bandari ya Kuingia
- Hudhibiti mipaka ya Canada
- Hupanga kukuondoa Canada ukipokea uamuzi hasi kwa madai yako ya ukimbizi
- Ina haki ya kukuweka kizuizini kama hawawezi kuthibitisha kitambulisho chako, kama wanaamini uhatari, au kama wanaamini hutazingatia sheria za uhamiaji Canada

Mawasiliano:

Library Square, 7th Floor
300 West Georgia Street
Vancouver BC V6B 6C9
Phone: 1-800-461-9999
Website: www.cbsa.asfc.gc.ca

Wizara ya Uhamiaji, Ukimbizi na Uraia Canada (IRCC)

- Huamua kama unaweza kufanya madai ya ukimbizi ukiwa nchini Canada
- Hufanya mchakato wa kibali cha kufanya kazi na bima ya afya inayosimamiwa na serikali (IFH) kwa mda

Mawasiliano:

1148 Hornby Street
Vancouver, BC V6Z 2C3

Phone: 1-888-242-2100
Website: www.cic.gc.ca

Piga simu kwa Msalaba Mwekundu ukiwa na maswali: 604-787-8858 au 1-866-771-8858

SWAHILI

MCHAKATO WA WANAODAI UKIMBIZI CANADA

Pata mwakilishi wa kisheria akusaidie kujaza fomu za ukimbizi na kwa hatua zote za mchakato wa ukimbizi. Ukiwa unahitaji usaidizi na hili, piga nambari ya simu ya Mawasiliano ya Kwanza na mtu wa kujitolea atakusaidia.

Kuna ratiba mbili kwa wanaodai ukimbizi wakiwa Canada. Chagua ratiba inayokuhusu:

Nilifanya madai ya ukimbizi katika Bandari ya Kuingia (uwanja wa ndege, mpaka wa nchi, bandarini) na Wakala wa Huduma ya Mpaka wa Canada (CBSA)

Siku ya 0

Kamilisha Mahojiano ya Kustahilishwa katika Bandari ya Kuingia.
Kama unastahili kufanya madai ya ukimbizi, utapokea vifuatavyo:

- Fomu ya Msingi wa Madai (BOC) itakayotakikana muda usiopita siku 15 kwa ofisi ya Bodi wa Uhamiaji na Ukimbizi
- Tarehe ya Masikizo yako ya Ukimbizi (ndani ya siku 45 kama unatoka Nchi Teule ya Asili (DCO), na ndani ya siku 60 kama unatoka nchi nyingine yoyote.

Siku ya 15

Wasilisha Fomu yako ya Msingi wa Madai kwa Bodi ya Uhamiaji na Ukimbizi

Nilfanya madai ya ukimbizi nchini Canada na Wizara ya Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia Canada (IRCC)- au nataka kufanya madai na

Siku ya 0

Enda kwa ofisi ya IRCC au pakua fomu za ukimbizi kutoka kwa mtandao wa intaneti: http://www.cic.gc.ca/english/refugees/inside/apply-how.asp

Enda ofisi ya IRCC na uwasilishe fomu zako. Wasili mapema (kabla ya saa nne za asubuhi) na uje na mkalimani kama huzungumzi Kiingereza au Kifaransa. Fomu zako zitakaguliwa na siku ya kuhojiwa kama unafaa, utapangwa kwa ratiba.

Hudhuria Mahojiano yako ya Kustahilishwa. Ikiwa umestahilishwa utapatiwa Tarehe ya Kusikizwa kabla ya siku 30 kwa Nchi Teule za Asili, na kabla ya siku 60 kwa Nchi Zisizo Teule za Asili.

Siku 10 kabla ya Masikizo yako

Wasilisha thibitisho lako kwa Bodi wa Uhamiaji na Ukimbizi

Siku ya 45 (Nchi Teule ya Asili) au Siku ya 60 (Nchi Isiyo Teule ya Asili)
Masikizo ya Ukimbizi mbele ya Bodi ya Uhamiaji na Ukimbizi

Siku ya 30 (Nchi Teule ya Asili) au Siku ya 60 (Nchi Isiyo Teule ya Asili)
Wasilisha thibitisho lako kwa Bodi ya Uhamiaji na Ukimbizi

Madai Yamekubaliwa

- Ikiwa waziri hajarufaisha uamuzi wako ndani ya siku 15, unaweza kutuma ombi la Makazi ya Kudumu kwa Wizara ya Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia Canada (IRCC)
- Ikiwa wewe ni Mteule wa Nchi ya Kigeni, itakubidi kungoja miaka 5 kabla ya kutuma ombi la Makazi ya Kudumu

Madai Yamekataliwa (Nchi Teule ya Asili na Nchi Isiyo Teule ya Asili)

- Tafuta msaada wa kisheria
- Tuma ombi ndani ya siku 15 kwa Idara ya Rufaa ya Wakimbizi (RAD)
- Tuma ombi la Tathmini ya Hatari Kabla ya Kuondolewa (PRRA)
- Tuma ombi la Misingi ya Kibinadamu na Huruma

Piga simu kwa Msalaba Mwekundu ikiwa una maswali: 604-787-8858 au 1-866-771-8858